



uia

MANIFESTO

KONGAMANO LA KIMATAIFA LA WABUNIFU MAJENGO
UIA 2023 COPENHAGEN
2-6 JULAI 2023

Mpango wa Kazi wa Makazi ya Jamii

Kwa ushirikiano wa Ubunifu wa Majengo na Watoto | Ubunifu wa Majengo kwa wote | Ubunifu wa Majengo wa Jamii na Haki za Binadamu | Maeneo ya Elimu na Utamaduni | Ubunifu wa Majengo, Miji, na Maeneo | Afya ya Umma | Maeneo ya Umma

MANIFESTO [Toleo 2.3]

Ubunifu wa Majengo wa Makazi ya Jamii: Yeyote Asiwachwe Nyuma

Kufuatia Azimio la Pamoja la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (1948), Kifungu 25.1, « Kila mtu ana haki ya kuishi kwa kiwango kinachotosheleza kwa afya na ustawi wake yeye mwenyewe na familia yake, ikiwa ni pamoja na chakula, nguo, na makazi na huduma za matibabu na huduma za kijamii zinazohitajika... » na Ajenda ya Makazi ya UN ya Mwaka 2030, tunathibitisha nia zifuatazo:

1. HAKI YA MAKAZI NI HAKI YA MAKAO

MAKAO | Makazi ni sehemu hai ya mazingira yaliyojengwa kwa ujumla na haki ya makazi ni haki ya makazi ya kina cha jumuiisha, afya, utamaduni na elimu na fursa za kijamii na kiuchumi yanayoheshimu mazingira. Kwa hivyo, makazi ni ya kudumu au ya muda (yenye nia ya kuwa ya muda na ya dharura ya kibinadamu) eneo la kibinafsi salama na lenye afya na maeneo ya kijumuiya na ya umma ambayo yanahitajika kwa maisha kamili kama makazi

2. HAKI YA MAKAO NI YA KILA MTU NA HAIWEZI KUONDOLEWA

MAKAZI YA JAMII | Kila mtu ana haki ya makazi ya jamii zinapaswa kuwa na dhamira ya kuitoa, kuhakikisha suluhisho la kutosha ili kutosheleza hitaji lililopingika, hata kwa watu wasiojiweza: Wanaoishi na ulemavu, wazazi wanaolea peke yao, wazee, wahamiaji, na maskini.

3. HAKI YA MAKAO INAWEZESHWA NA UBUNIFU WA MAJENGO

UBUNIFU WA MAJENGO WA MAKAZI YA JAMII | Ubunifu wa majengo ni mwakilishi wa jamii katika kubuni makazi ya kijamii yanayojumuisha wote, ambayo lazima yatimize mahitaji yote ya binadamu na uwezo wake, na kuhakikisha angalau haki za chini kama (lakini sio chini ya) makazi yanayoweza kumudu.

Ili makazi yawe ya kijamii yanayojumuisha wote, sio tu nyumba, bali pia suluhisho zenye hadhi, za kudumu kwa muda mrefu, na zenye afya, huku kuhakikisha wakati huohuo faragha na utu binafsi kwa wakazi. Kwa hivyo, makazi yanapaswa kujengwa juu ya nguzo nne muhimu:

1. MAKAO KAMA NYUMBA

HESHIMA | Kubuni makazi bora, ni lazima yawe yamepangwa kuhakikisha pia kiwango cha chini cha kuwepo kwa ubora na siyo tu kiwango cha chini cha ukubwa. Zaidi ya hayo, nyumba (hasa zile zenye gharama nafuu) hazipaswi kuwa na unyanyapaa, bali zijengwe vizuri, ziliingane na kuzingatia mazingira yake.

2. MAKAO KAMA KIINI

USHIRIKISHWAJI NA USHIRIKIANO | Kubuni makazi yanayojaa shughuli na yenye uhai, ni lazima yafikiriwe kama mfumo wa miundo mbinu ya nafasi na makazi, huambatana na mchakato wa usanifu wa kujumuisha na mfumo wa kina ambapo watu wanaweza kuishi na kushiriki, kubuni makazi yao kulingana na mahitaji, matakwa, na uwezo wao. Hivyo basi, makazi ya kijamii si suluhisho lililopangwa mapema, bali ni kazi endelevu ambapo wakazi wanaweza kuongeza kiini kilichotolewa kadri ya wakati, kubadilisha upya makazi yao pamoja na nafasi za faragha au za kushirikishana, ndani na nje.

3. MAKAO KAMA KIUMBE HAI

UJUMUISHAJI WA MIJI | Kubuni makazi ya kijamii yanayojumuisha wote, ni lazima iepuke kujitenga na kutenganisha: lazima yajumuishe makazi, maeneo ya umma, na miundombinu. Badala ya makazi yaliyotengwa na yaliyo nje ya miji, ni lazima kupangwa makazi yaliyojumuishwa ndani ya mazingira ya mjini: mfumo wa maeneo mengi ya kijani, vituo vya kulelea watoto, na shule, maduka, majengo ya kitamaduni na kidini, miundombinu ya michezo, usafiri wa umma, n.k. lazima uhakikishwe na uwezeshwe kwa kila mtu

4. MAKAO KAMA MCHAKATO WA KUJIBU WITO

UTUNZAJI WA MIZINGIRA | Kubuni makazi ya kijamii ya heshima kwa siku za usoni, ni lazima pia yawe endelevu, yakihakikisha misingi ya uwezekano na mazingira: sehemu ya kwanza kutoka maoni ya kiuchumi, kijamii, na kiufundi; sehemu ya pili kwa kubuni kwa kuzingatia matumizi ya nishati na uhifadhi wa maisha ya asili, lakini pia kutumia vifaa vya ujenzi vinavyoweza kurejelewa na vile vya eneo hilo na mbinu zinazoruhusu watu kushiriki katika uchumi, kuunda vitu wenyewe na kuvitangaza, kuwa sehemu ya mfumo mpana na maisha ya jamii

Tunatoa wito kwa nguvu kwa wale wote wanaofanya maamuzi katika mamlaka yaserikali, wajasiriamali wa umma na binafsi, wataalamu walioboea katika sekta husika, na wenzetu katika taaluma ya Ubunifu wa majengo, kuchukua - vilevile umma kwa ujumla kudai - kanuni za tamko hili